

## **Zuia Huo Ulimi!**

Kuna mtu alisema "Chunga ulimi wako maana uko katika sehemu iliyolowana na ni kama unaelekea kuteleza" ni mara ngapi ulimi wako umeteleza? Ni mara ngapi umeongea jambo ambalo lilipotoka ultamani ungeweza kulirudisha kinyawani? Ndiyo maana katika Yakobo 1:19 twaambiwa ya kwamba "...Basi kila mtu awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika." Kwa hakika, namna tunavyozizua ndimi zetu siku hizi hufanya dini yetu kuthibitika. Maana katika Yakobo 1:26 Biblia Yasema "Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyoni mwake, dini yake mtu huyo haifai." Maana ya Yakobo hapa iko dhahiri. Unawezakuwa mwaminifu kuhudhuria vipindi vya ibada, kuimba sifa kama malaika, kuinamisha kichwa wakati wa sala na kutoa sana kama vile mjane na senti. Lakini endapo unashindwa kuuzuia ulimi wako, basi uko katika hatari ya kutofaa.

Leo hakuna mtu anayetaka kuwa wa hovyo. Tunataka kuaminika, tunataka watu watuamini na tunataka kuonekana wakweli. Na tunaweza kuwa hivyo, kama tutakuwa "wepesi wa kisikia, bali si wepesi wa kusema" Katika Mithali 25:19 Biblia inasema "Kumtumaini asiye mwaminifu wakati wa taabu ni kama jino lililovunjika, au mguu ulioteguka". Fungu hili nimeona linavutia sana. Hivi, ni nani anayeweza kulitumaini jino lililovunjika wakati wa kula? Nani anaweza kuutumaini mguu uliovunjika wakati wa kushuka kwenye ngazi ya ndege? Hakuna! Leo kama unataka uonekane wa kuaminiwa, basi unahitahitaji kuuzuia ulimi wako!

Ukweli ni kwamba siri zinatakiwa kubaki siri! Zibaki kama hela zinavyohifadhiwa kwenye sanduku la kutunzia hela benki ili zisitolewe. Ukitoa, juu kwamba siri zako zitapaa na hakuna kitakachozizua. Muhubiri 10:20 " Usimlaani mfalme, la, hata katika wazo lako; wala usiwalaani wakwasi chumbani mwako kwa kuwa ndege wa anga ataichukua sauti, na mwenye mabawa ataitoa habari."

Unataka kujulikana kama wa kutumainiwa mwaminifu? Unataka watu wakutumaini? Unataka wanaokuzunguka waendelee kukutumaini? Basi tii tu maagizo aliyokupa Bwana. Sikiliza na hifadhi unachosikia katikati ya masikio yako! Uzuie huo ulimi. Na yote yatakunyookea!